# NATIONAL RECONSTRUCTION ALLIANCE

# N.R.A

## KATIBA YA CHAMA

Toleo la 1-2017

# SOMO LA KWANZA

## IJUE NATIONAL RECONSTRUCTION ALLIANCE (N.R.A)

## UTANGULIZI.

Kwa mujibu wa sheria Na.5 ya mwaka 1992,N.R.A ni chama cha kisiasa,chenye usajili wa kudumu, kilichopata usajili wake tarehe 8/2/1993 na kupata namba ya Usjili No.00009.

### MAUDHUI YA ALAMA ZA CHAMA.

### I. BENDERA.

Bendera ya N.R.A ina rangi tatu.**Nyekundu,Nyeupe na Nyeusi** na alama nyingine mbili zinazoonekana katika Bendera ,Alama hizo ni **Ufagio** na **Jua linalochomoza**.

### II. TAFSIRI YA RANGI ZA BENDERA.

**(a) <u>NYEKUNDU.</u>**
Hii maana yake ni ishara ya kumbukumbu ya wale wote waliokufa,waliomwaga damu yao kwa ajili ya ukombozi wa nchi hii,Mashujaa ambao hufanyiwa kumbukumbu kitaifa kila mwaka katika jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

(b) <u>NYEUPE.</u>
Hii maana yake ni ishara ya kwamba tunahitaji sana amani katika Jumhuri yetu ya Muungano wa Tanzania na kwamba N.R.A itasimamia kwa gharama yoyote kuweka amani nchini.Hali kadhalika hii ni ishara ya kuweka matumaini.

(c) <u>NYEUSI.</u>
Rangi hii ina maana ya kuashiria bara la Afrika na Waafrika.Hii ni kuonyesha kwamba shughuli na harakati za N.R.A zinafanyika katika bara la Waafrika.

## III. UFAGIO NA JUA LINALOCHOMOZA.

### A. <u>JUA LINALOCHOMOZA.</u>

Jua hili linaonekana kuchomoza asubuhi.Hii ni ishara kwamba sasa kumepambazuka au kumekucha,Jua ni ishara ya mwanga unaoondoa giza,yaani baada ya wananchi kudhulumiwa kwa namna moja au nyingine N.R.A sasa inawaletea matumaini mapya.

### B. UFAGIO

Hii ni ishara kwamba kila kunapopambazuka watu huanza shughuli za kusafisha mazingira ya nyumba , ofisi zao ama sehemu zingine za kazi.

Kwa mantiki hiyo ya alama za N.R.A ni kuwa;
N.R.A kwa upande wake inayaona mabadiliko yanayohitaji kwa wananchi ni lazima kwanza wawekwe bayana ili yajulikane.

Giza lililowekwa ili mabaya yasionekane lazima liondolewe kila pahala palipojificha maovu.Kwa hali hii "JUA" ndio mwanga unaohitajika kuangaza safari yetu ya kuleta maendeleo na kujenga jamii bora.

Mwanga huo unaashiria UWAZI katika uendeshaji wa shughuli na harakati za N.R.A. Baada ya kuyaona maovu yote yaliyopo ndani ya jamii naTaifa kwa ujumla ni lazima kuyaondoa kwa kuyafagia.

Hivyo basi Alama ya **"UFAGIO"** ni ishara mahsusi na imesimama hapa kama nyenzo ya kuyaondoa au kuyafagia maovu hayo yanayoonekana katika Mifumo ya nchi,Sera,sheria na Taratibu mzima za uendeshaji wa shughuli za Serikali na vyombo vyake katika nchi.

## SOMO LA PILI.

### I. MAUDHUI YA KAULI MBIYU ZA CHAMA.

**A.** Kauli mbiyu zinatokana na alama za chama kama zilivyoelezwa na zitatamkwa au kutolewa salamu na muitikio wake utakuwa kama ifuatavyo;

(Jedwari 1)

| MATAMKO YA KAULI MBIYU | MUITIKIO WA KAULI MBIYU |
|---|---|
| **N.R.A** | MWAMKO WA UMMA |
| **JUA** | KUMEPAMBAZUKA |
| **FAGIO** | KUONDOA MAOVU |
| **TAIFA KWANZA** | VYAMA BAADAE |

### B. UTARATIBU WA KUSALIMIANA NA ALAMA ZAKE.

N.R.A itatumia alama ya NGUMI wakati wa kutoa salamu za chama kwa kauli mbiyu.Utaonyesha mkono wa kulia na kuupandisha juu wakati unasema **N.R.A ,JUA** na **FAGIO,TAIFA KWANZA.**

## C. MISINGI MIKUU YA CHAMA CHA N.R.A

(Jedwari 2)

| MISINGI YA CHAMA NA MAELEKEZO YAKE KWA UFUPI | |
|---|---|
| **UHURU** | Hapa inamaanisha uhuru wa kuabudu, kuishi,habari,kujieleza,kujiunga,uhuru wa kiuchumi,kifikra,uhuru dhidi ya shinikizo za Ukoloni na ukoloni mamboleo |
| **HAKI** | Haki za kisheria,kuchagua,kuchaguliwa,kuishi,kusikilizwa,kuwa na serikali yenye utawala wa kisheria,haki ya kulindwa dhidi ya dhulma,uonevu,udikteta,haki za usawa wa kibinadamu,haki za elimu,kusafiri,haki za kuheshimiwa,demokrasia n.k |
| **AMANI** | Uhuru na haki vikipatikana"AMANI" itazaliwa,kila mtu atakuwa huru na kupewa haki yake,hivyo AMANI itashamiri katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania |
| **USAWA** | Usawa kwa jamii nzima ni jambo la msingi kwa uswawi wa Taifa letu, watu wote ndani ya Taifa bila kujali itikadi zao,Rangi,Dini,uwezo wao NRA inawaona ni sawa mbele za sheria ,vyombo na mifumo mingine ya dola. |
| **UMOJA** | Umoja utapatikana pale penye UHURU na HAKI, AMANI na USAWA.<br>Upendo ndani ya jamii utapata nafasi yake kwani kutakuwa hakuna dharau,ubaguzi,dhuluma,ukandamizaji n.k |
| **MAENDELEO** | Dhana ya Uhuru , Haki , Amani , Usawa na Umoja vikipatikana ndani ya jamii,mazingira ya kupatikana kwa MAENDELEO yatakuwa yatajengeka. |
| *Hivyo N.R.A inaona kuwa **UHURU,HAKI, AMANI ,USAWA na UMOJA WA TAIFA ni** hazina yenye kubeba uhai wa Taifa na isiyofaa kuchezewa na mtu,chama ama kundi lolote la nje au ndani ya Taifa hili.*<br><br>*Na ndio maana N.R.A tusema **TAIFA KWANZA, VYAMA BAADAE*** | |

## SEHEMU YA KWANZA.

### 1. JINA, LUGHA NA MAKAO MAKUU YA CHAMA.

**a) JINA LA CHAMA.**

Jina la chama litakuwa National Reconstruction Alliance kwa kifupi N.R.A.
Jina hili halitabadilishwa au kutafsiriwa kwa lugha nyingine yoyote.

**b) LUGHA.**

Lugha rasmi ya chama ni Kiswahili.Lakini Lugha nyingine yoyote yaweza pia kutumika kwa maslahi ya chama.

### 2. MAKAO MAKUU YA CHAMA.

(a) Ofisi Kuu na Makao Makuu ya chama yatakuwa ***DAR-ES – SALAAM***

(b) Ofisi ndogo ya Makao Makuu itakuwa Zanzibar (Itaitwa Makao Makuu Ndogo).

## SEHEMU YA PILI.

### 3. ALAMA YA CHAMA.

Chama kitakuwa na alama au nembo mbalimbali zilizopitishwa na kukubaliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa, nazo ni:-

(a) Jua linalochomoza
(b) Fagio

### 4. MAANA YA NEMBO ZA CHAMA.

(a) **Jua linalochomoza**, hili linaonekana kuchomoza asubuhi.Hii ni ishara kwamba sasa kumepambazuka au kumekucha,Jua ni ishara ya mwanga unaoondoa giza,yaani baada ya wananchi kudhulumiwa kwa namna moja au nyingine N.R.A sasa inawaletea matumaini mapya.

(b) **Fagio,** maana yake ni kwamba,kwa kuwa kumekucha jambo la kwanza ni kusafisha mazingira,hivyo fagio litamaanisha kuondoa maovu yote katika jamii.

### 5. BENDERA YA CHAMA.

Chama kitakuwa na bendera yenye rangi tatu.

(a) Nyekundu
(b) Nyeupe
(c) Nyeusi

### 6. MAANA YA RANGI HIZI.

a) Nyekundu inamaanisha kumbukumbu ya Watanzania wote waliopoteza maisha yao katika kupigania Uhuru,haki,usawa,amani na maendeleo ya Taifa hili kama historia inavyoonyesha.

b) Nyeupe inaonyesha amani na utulivu ambao chama kinataka kudumisha, kuitanua na kuimarisha zaidi.
c) Nyeusi ni alama ya rangi asilia ya wananchi wa Jamhuri ya Tanzania na Bara Zima la Afrika.

## SEHEMU YA TATU.
## IMANI NA MADHUMUNI YA CHAMA.

### 7. IMANI YA CHAMA.

(a) Chama kinaamini katika uwepo wa Mungu mwenye mamlaka yote ya Dunia na ndiye mwenye nguvu zote na anayemiliki mbingu na ardhi.
(b) Chama kinaamini katika falsafa ya utu na haki za binaadamu.
(c) Chama kinaamini katika maamuzi ya walio wengi na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ambayo kwayo tija kwa wote itapatikana.
(d) Chama kinaamini kuwa elimu ni haki kwa kila mtu.
(e) Chama kinaamini katika uchumi wa soko huria lenye tija kwa Watanzania.
(f) Chama kinaamini katika mahusiano bora na yenye manufaa kati ya mtu na mtu na vikundi mbali mbali vyenye itikadi tofauti.
(g) Chama kinaamini katika utawala wa kisheria.
(h) Chama kinaamini kwamba bila ya **UHURU** hakuna **HAKI** bila ya haki hakuna **AMANI** na bila ya amani hakuna **UMOJA** na bila ya umoja hakuna **MAENDELEO.** Kwahivyo Chama kitafuata falsafa ya *mlengo wa Kati usiofungamana na upande wowote.*

### 8. MADHUMUNI YA CHAMA.

(a) kushika dola na kuweka sera madhubuti ya utoaji wa elimu kwa watu wote.
(b) Kuweka sera madhubuti zitakazo ondoa matabaka katika jamii. Mfano tabaka la wenye wenye nacho na wasio nacho, wenye elimu na wasio na elimu, waugwana na watwana.
(c) Kudumisha heshima ya utu na ubinaadamu, kupambana na nguvu zozote zenye lengo la kumdhalilisha binaadamu.
(d) Kulinda na kudumisha uhuru na Muungano wa Watanzania na kuhakikisha kuwa serikali inayotawala ni ya kidemokrasia na itendayo haki kwa watu wote.
(e) Kuhakikisha kuwa serikali inashiriki na kuwashirikisha watu wake kikamilifu kwa kila hali ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.
(f) Kuhakikisha kuwa serikali inaondoa dhuluma miongoni mwa raia zake, ubaguzi, udini, ukanda , rushwa, ubadhirifu, wizi wa mali ya umma, unyang'anyi na maovu yote kwa ***dhati ya matendo*** na wala si kwa maneno tu au maandishi.
(g) kuhakikish Chama kinashirikiana na mtu yeyote au kikundi chochote chenye lengo la kusaidia katika kufikia na kutekeleza azma hizi.

## SEHEMU YA NNE.
## UANACHMA.

**9. SIFA ZA MWANACHMA.**

(a) Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane (18).
(b) Awe na akili timamu.
(c) Asiwe Mwanachama wa chama kingine cha Siasa.
(d) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa ama kuandikishwa kisheria.
(e) Asiwe mpenda makuu, mbadhilifu, mzinzi, mnyanyasaji, dhulumati, mwizi, kwa kifupi awe mtu muadilifu.

**10. WAJIBU WA MWANACHAMA.**

(a) Awe mtiifu kwa chama.
(b) Awe tayari kukisaidia chama
(c) Aielewe, aieleze na kuitetea katiba na sera za chama
(d) Aepukene na tabia ya kung'ang'ania madaraka
(e) Alipe kiingilio na ada za uwanachama.

**11. HAKI ZA MWANACHAMA.**

(a) Mwanachama anayo haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika nafasi yoyote ya uongozi.
(b) Kukosoa na kukosolewa

**12. MWISHO WA UWANACHAMA.**

i. Kufariki dunia
ii. Endapo atapoteza sifa za uwanachama
iii. kujiuuzulu au kufukuzwa uanachama.

## SEHEMU YA TANO.

**13. MUUNDO WA CHAMA.**

Chama kitakuwa na muundo ufuataο:-

(a) Mkutano Mkuu
(b) Kamati kuu ya utendaji ya chama
(c) Halmashauri kuu ya taifa **(HAKUTA)**
(d) Baraza la ushauri la wazee.

**14. UONGOZI WA CHAMA**

i. Ngazi za uongozi katika chama zitakuwa kama ifuatvyo;

(a) Uongozi wa chama Taifa
(b) Uongozi wa chama Mkoa
(c) Uongozi wa chama Wilaya
(d) Uongozi wa chama Kata
(e) Uongozi wa chama Tawi

**15. MUUNDO WA UONGOZI.**

Muundo wa nafasi za uongozi katika chama utafuata mtitiriko wa muundo wa chama uliotajwa katika sehemu ya Tano ,ibara ya 14(a,b,c,d,e)

**16. VIONGOZI WA CHAMA.**

i. Chama kitakuwa na viongozi kama walivyotajwa katika sehemu ya Tano ,ibara ya 14(a,b,c,d,e)

ii. Makao makuu ya chama yatakuwa na viongozi wafuatao;

a. Mwenyekiti wa Taifa
b. Makamu Mwenyekiti Bara
c. Makamu Mwenyekiti Zanzibar
d. Katibu Mkuu Taifa
e. Naibu Katibu Mkuu Bara
f. Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
g. Katibu Mwenezi Taifa
h. Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Taifa
i. Katibu wa Bodi ya Wadhamini Taifa
j. Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini
k. Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Taifa
l. Katibu wa Baraza la Wazee Taifa
m. Wajumbe wa Baraza la wazee
n. Wakuu wa Kurugenzi za chama Taifa

**17. KURUGENZI ZA CHAMA TAIFA.**

a. Chama kitakuwa na kurugenzi mbali mbali katika ofisi za uongozi wa chama, Kurugenzi za chama zitakuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu , ambazo ni kama zifuatazo:-

i. Elimu na Ushirikishwaji
ii. Uenezi na Uhamasishaji
iii. Mambo ya nje , Bunge ,Mahusiano na Ushirikiano wa Kimataifa
iv. Vijana, Mila, Desturi,Tamaduni na Michezo
v. Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake , Jinsia na Watoto
vi. Uchumi,Sera, Mipango na Maendeleo ya Wafanyakazi
vii. Utafiti, Afya na Mazingira
viii. Itifaki na Nidhamu
ix. Habari, Nyaraka na Takwimu
x. Sheria na Haki za Binaadamu
xi. Uchaguzi na Uratibu
xii. Walemavu (Watu wenye mahitaji Maalum)
xiii. Mawasiliano,Sayansi na TEKNOHAMA
xiv. Fedha.
xv. Vyuo Vikuu.
xvi. Watanzania Waishio Nje ya Tanzania

b. Isipokuwa tu, kurugenzi ya fedha itaanzia kwenye tawi.

c. Bila kuathiri kifungu cha 17(a), Kurugenzi hizi zinaweza kuwa kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa na ofisi ndogo ya makao makuu Zanzibar.
d. Kamati kuu ya utendaji ambao mwenyekiti wake wa chama Taifa, ndiye mwenye mamlaka ya mwisho kuongeza, kubadili au kupunguza kurugenzi hizi baada ya kushauriana na kukubaliana na wasaidizi wake na katibu wake mkuu.

## SEHEMU YA SITA.
## NAMNA YA KUPATA VIONGOZI WA CHAMA.

### 18. VIONGOZI WA TAWI.

a. Tawi linaundwa na wanachama wasipungua kumi (10)
b. Viongozi wa tawi watachaguliwa na mkutano mkuu wa tawi.
c. Watakaochaguliwa ni:-
   i. Mwenyekiti.
   ii. Makamu mwenyekiti.
   iii. Katibu.
   iv. Mweka Hazina
   v. Wajumbe watano (5) watakaoingia kwenye mkutano mkuu wa kata wakizingatia uwepo ya uwakilishi wa kijinsia,rika au watu wenye ulemavu.

d. Wajumbe wa mkutano wa tawi watakuwa wanachama wote walioko kwenye tawi.
e. Viongozi wa ngazi za juu wa chama walioko katika tawi wanayo haki ya kuhudhuria vikao lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura ama kupigiwa kura.
f. Mwenyekiti na katibu wa baraza la ushauri la Wazee wa Tawi

### 19. VIONGOZI WA KATA.

a. Kata itaundwa na matawi kuanzia mawili (2) yaliyoko kwenye kata hiyo.
b. Viongozi wa kata watachaguliwa na mkutano mkuu wa kata.
c. Watakao chaguliwa namkutano mkuu wa kata ni :-
   i. Mwenyekiti
   ii. Makamu mwenyekiti
   iii. Katibu
   iv. Mweka Hazina
   v. Wajumbe watatu (3) watakaoiwakilisha kata katika mkutano mkuu wa wilaya
   vi. Mjumbe mmoja (1) wa halmashauri ya wilaya (w)
   vii. Mwenyekiti na katibu wa baraza la ushauri la Wazee la kata.

d. Wajumbe wa mkutano mkuu wa kata ni :-
   i. Viongozi wa matawi.
   ii. Viongozi wa ngazi za juu waliopo kwenye kata hiyo ,hawa wanayo haki ya kuhudhuria vikao vya kata, lakini hawataruhusiwa kupiga ama kupigiwa kura.
   iii. Wajumbe watano (5) kutoka kila tawi.
   iv. Viongozi wa kata husika.

**20. VIONGOZI WA WILAYA.**

a. Wilaya itandwa kutokana na kata zilizoko kwenye wilaya hiyo.
b. Viongozi wote wa Wilaya watachaguliwa na mkutano mkuu wa Wilaya
c. Watakaochaguliwa na mkutano mkuu wa wilaya ni hawa wafuatao:-
   i. Mwenyekiti
   ii. Makamu Mwenyekiti
   iii. Katibu
   iv. Mjumbe mmoja (1) wa halmashauri ya mkoa
   v. Mwenyekiti na katibu wa baraza la ushauri la Wazee la wilaya.

d. Wajumbe wa mkutano mkuu wa Wilaya ni:-
   i. Viongozi wote wa Wilaya.
   ii. Viongozi wote wa kata
   iii. Viongozi wa ngazi za juu walioko katika Wilaya ambao watahudhuria vikao lakini hawataruhusiwa kupiga ama kupigiwa kura.
   iv. Mwenyekiti na katibu wa baraza la ushauri la Wazee la Kata

**21. VIONGOZI WA MKOA.**

a. Mkoa utaundwa kutokana na Wilaya zote zilizoko kwenye Mkoa huo
b. Viongozi wa mkoa watakaochaguliwa na mkutano mkuu wa mkoa ni:-
   i. Mwenyekiti
   ii. Makamu Mwenyekiti
   iii. Katibu
   iv. Mweka Hazina
   v. Wajumbe mmoja (3) wa mkutano mkuu wa Taifa ,ambapo mmoja sharti awe mwanamke.
   vi. Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wazee la mkoa.

c. Wajumbe wa Mkutano mkuu wa Mkoa watakua hawa wafuatao:-
   i. viongozi wote wa Mkoa.
   ii. Viongozi wa Wilaya.
   iii. Viongozi wa ngazi za juu walioko katika mkoa
   iv. Mjumbe mmoja (1) aliyechaguliwa katika mkutano wa wilaya.

**22. VIONGOZI WA KITAIFA.**

(a) Taifa litajumuisha mikoa yote iliyoko nchini
(b) Mkutano mkuu wa taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:-

   i. Mwenyekiti
   ii. Makamu Bara na Visiwani.
   iii. Katibu Mkuu Taifa
   iv. Naibu katibu mkuu bara na Visiwani.
   v. Viongozi wote wa makao makuu ya chama bara na Zanzibar
   vi. Wenyeviti na makatibu wote wa mikoa
   vii. Mjumbe mmoja (1) mwanamke kutoka kila mkoa
   viii. Mwenyekiti na katibu wa baraza la wazee taifa na wajumbe wao

ix. Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wadhamini wa Chama na wajumbe wao

(c) Viongozi wa kitaifa watakaochaguliwa na mkutano mkuu wa Taifa ni;

i. Mwenyekiti Taifa
ii. Makamu mwenyekiti Bara
iii. Makamu mwenyekiti Zanzibar
iv. Katibu mkuu Taifa
v. Mwenyekiti Baraza la Wazee
vi. Katibu Baraza la Wazee
vii. Mwenyekiti Bodi ya chama
viii. Katibu Bodi ya chama.
ix. *Bila ya kuathiri kifungu c(i-viii)* ***Mwenyekiti na Katibu Mkuu*** *watatoka pande mbili za Muungano, Iwapo Mwenyekiti atatoka Bara Katibu Mkuu atatoka Zanzibar, na endapo Mwenyekiti atatoka Zanzibar Katibu Mkuu atatoka Bara.*

## 23. VIONGOZI WA KUTEULIWA

a. Kutakua na viongozi wa kitaifa wa kuteuliwa,ambao ni wafuatao:-
i. Naibu katibu Mkuu Bara.
ii. Naibu Katibu Mkuu Zanzibar
iii. Katibu Mwenezi
iv. Wajumbe wa Bodi ya Wadhamin
v. Wajumbe wa Baraza la Wazee
vi. Wakuu wa Wakurugenzi.

b. **Namna ya kufanya uteuzi.**
Viongozi wote wa kitaifa wa kuteuliwa watateuliwa na Mwenyekiti wa chama Taifa aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa uchaguzi baada ya kushauriana na wasaidizi wake na Katibu mkuu wa chama.

c. Kabla ya Uteuzi, Majina ya viongozi hao yatapendekezwa ,kujadiliwa,kuchujwa na kupitishwa na vyombo vya chama.

d. **Namna ya kutengua uteuzi.**
Mwenyekiti wa chama Taifa aliyechaguliwa na mkutano mkuu wa uchaguzi ndiye mwenye mamlaka ya kutengua uteuzi wa viongozi wa kuteuliwa baada ya kutimiza masharti ya vikao vya Mabaraza mbalimbali.

## 24. MUDA WA UONGOZI MADARAKANI.

i. Viongozi wote wa kuchaguliwa na kuteuliwa na chama ,watakaa madarakani kwa muda wa miaka mitano(5)
ii. Uongozi utachaguliwa katika uchaguzi huru wa kidemokrasia.

## SEHEMU YA SABA.
## VIKAO VYA CHAMA.

**25. VIKAO VYA TAIFA.**

i. Kutakua na mkutano mkuu wa Taifa mara moja (1) baada ya miaka mitano (5)
ii. Huu ndio mkutano mkuu wa uchaguzi.
iii. Kamati kuu ya utendaji itakutana mara moja (1) kila mwezi.
iv. Halmashauri kuu ya chama itakutana mara moja (1) kwa mwaka.
v. Mkutano wa dharura waweza kuitishwa katika ngazi yoyote iwapo italazimika kufanya hivyo.
vi. Kila kikao kitalazimika kuwa nanusu (1/2) ya wajumbe wote.
vii. Mikutano yote itakua chini ya uongozi wa Mwenyekiti na Katibu mkuu.
viii. Mwenyekiti Taifa ndiye atakayeitisha mikutano yote ya Kitaifa baada ya kushauriana na wasaidizi na Katibu wake mkuu.
ix. Endapo Mwenyekiti na Katibu watashindwa kwa sababu moja au nyingine kuitisha mkutano, Mwenyekiti wa Baraza la wazee ataitisha mkutano, Mwenyekiti wa Baraza la wazee ataitisha mkutano baada ya kupokea maombi yenye saini kutoka kwa theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote. Mahtasari wa kikao hicho utapelekwa kwenye ngazi ya juu ya utendaji.
x. Muda wa taarifa wa kuitisha kikao cha kawaida usiwe chini ya siku kumi na nne (14).

**26. VIKAO VYA MKOA.**

(a) Kamati ya utendaji ya mkoa itakutana mara moja (1) kila mwezi

(b) Halmashauri kuu ya mkoa itakutana kila baada ya miezi sita (6).

**27. VIKAO VYA WILAYA.**

(a) Kamati ya utendaji itakutana mara moja (1) kila mwezi

(b) Halmashauri kuu ya wilaya itakutana mara moja(1) kila baada ya miezi mitatu (3)

**28. VIKAO VYA KATA.**

(a) Kamati ya utendaji itakutana mara moja (1) kila mwezi

(b) Halmashauri ya kata itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi miwili (2)

**29. VIKAO VYA TAWI.**

(a) Kamati ya utendaji itakutana mara moja (1) kila mwezi
(b) Halmashauri ya tawi itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi miwili (2)

## SEHEMU YA NANE
## MAJUKUMU NA KAZI ZA VIKAO VYA CHAMA.

### 30. MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA TAIFA.

(a) Mkutano mkuu wa chama Taifa unayo majukumu yafuatayo;

i. Kuchagua viongozi wa Kitaifa
ii. Kupokea taarifa ya shughuli za chama kutoka Halmashauri kuu na kujadili
iii. Kupitisha, kuthibitisha, kuchunguza na kutoa maagizo ya mambo yote ya chama
iv. Kuhakiki mahesabu,sera na miongozo mingine.
v. Kutoa maamuzi juu ya jambo lolote la chama, kubadili, kupendekeza au kurekebisha kifungu chohote cha katiba, kanuni ama sera ya chama.

### 31. HALMASHAURI KUU YA TAIFA.

(a) Halmashauri kuu ya Taifa itakua na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti na Makamu wawili Bara na Zanzibar
ii. Katibu Mkuu Taifa na Naibu Bara na Zanzibar
iii. Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wazee
iv. Mjumbe mmoja (1) kutoka kila mkoa, mwenyekiti au mwakilishi wake.

### 32. MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU TAIFA.

(a) Halmashauri kuu Taifa inayo majukumu yafuatayo;

i. Kupokea maagizo na kuyafanyiwa kazi kutoka mkutano mkuu.
ii. Kupokea taarifa za kazi za chama kutoka kamati kuu ya utendaji na kuzifanyia maamuzi.
iii. Kusimamia, kufuatilia ,kuongoza shughuli,Tabia na mienendo ya viongozi watendaji wa chama.
iv. Kufanya kazi zingine zote kama zitakavyoagizwa na mkutano mkuu.
v. Kuandaa agenda za mkutano mkuu kama zitakavyopendekezwa na baraza la utendaji la Halmashauri kuu.
vi. Kutengeneza sera, sheria, ndogo ndogo na miongozo mingine ndani ya chama.

### 33. KAMATI KUU YA UTENDAJI.

(a) Kamati kuu ya Utendaji ina Wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti na Makamu wake wawili
ii. Katibu Mkuu na Manaibu wake wawili
iii. Wakurugenzi wote wa chama.

### 34. MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA UTENDAJI.

(a) Kupokea maagizo na kufanyia kazi kutoka **HAKUTA**
(b) Kutenda shughuli zote za kila siku za chama
(c) Kuweka, kubuni na kupanga mikakati ya ushindi
(d) Kupendekeza kwa halmashauri kuu ya taifa mambo yote yanayohitaji baraka za HAKUTA
(e) Kuratibu na kufuatilia shughuli zote za chama, uchaguzi, kampeni, uenezi, propaganda na yote mengine.

(f) Kufanyia kazi mambo yote kama yatakavyoelezwa na Mwenyekiti na katibu mkuu
(g) Kuziba naafasi ya kiongozi yeyote iliyoachwa wazi kwa sababu yeyote ile baada ya kutimiza robo tatu(3/4) ya kura za wajumbe wote
(h) Bila kuathiri kifungu (g), Baraza la Wazee na Bodi ya Wadhamini watahusika katika jukumu (g) ili kufanikisha ufanisi wa maamuzi ya kikao hihi kwa manufaa ya chama.

**35. BARAZA LA USHAURI LA WAZEE.**

(a) Kutakuwa na Baraza la Ushauri la Wazee,wajumbe wa Baraza hili ni:-
  i. Mwenyekiti na Katibu wake watakaochaguliwa na mkutano mkuu Taifa.
  ii. Wajumbe watano (5) watakaoteuliwa na kamati kuu ya utendaji wa chama.
  iii. Miongoni mwao Wajumbe watatu (3) watakuwa wanawake.

**36. MAJUKUMU YA BARAZA LA USHAURI LA WAZEE.**

(a) Kushauri na kukemea juu ya mienendo na tabia za viongozi zenye mielekeo ya kwenda kinyume na miiko ya uongozi kwa kukiuka katiba au sera ya chama.
(b) Walinzi wa umoja, amani, usalama, katiba na sera ndani ya chama.
(c) Kutenda kazi kama tume ya uchunguzi kuhusu tabia za viongozi ndani ya chama.
(d) Walinzi wa demokrasia ya kweli ndani ya chama.
(e) Kuitisha mikutano ya wazee wote na Mkutano wowote wa kitaifa pale ambapo Mwenyekiti au Katibu Mkuu watakaposhindwa kufanya hivyo.

**37. SIFA YA KUWA MWANABARAZA.**

(a) Baraza la wazee litakuwa na wajumbe wenye umri usiopungua miaka hamsini (50).
(b) Asiwe mbinafsi, mnyanyasaji, dhulumati, mbadhirifu, mzinzi, mwizi, kwa kifupi awe mtu muadilifu.

## SEHEMU YA TISA.

## MAJUKUMU YA VIONGOZI WA CHAMA.

**38. MWENYEKITI WA CHAMA TAIFA.**

(a) Atakuwa Mkuu wa chama na msemaji mkuu
(b) Ataongoza na kusimamia miongozo yote ya chama.
(c) Atakuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya kitaifa na muitishaji wa vikao hivyo.
(d) Atakuwa na kauli ya mwisho katika masuala yote ya kiutawala na uendeshaji baada ya kushauriana na wasaidizi na watendaji wake
(e) Msimamizi mkuu na mlinzi mkuu wa katiba na sera za chama.
(f) Katika kutumia uwezo wake wa kikatiba mwenyekiti atawashirikisha wasaidizi wake na Kaibu mkuu wa chama na vyombo vingine vya chama ili kufikia maamuzi sahihi.

**39. MAKAMU MWENYEKITI.**

(a) Makamu mwenyekiti atakaimu majukumu ya mwenyekiti atakapokuwa hayupo.

(b) Mshauri mkuu wa mwenyekiti na msaidizi wa kazi zote za mwenyekiti za kila siku.

**40. KATIBU MKUU.**

(a) Mkuu wa shughuli za kisekretariati katika chama

(b) Mtendaji mkuu wa shughuli zote za kiutendaji za chama

(c) Kutunza kumbukumbu, mihutasari ya vikao na kusambaza taarifa za chama.

(d) Katika utendaji wake wa shughuli za chama atawajibika kwa mwenyekiti .

(e) Msimamizi na Mshauri mkuu wa kazi zote za utendaji za chama kwa mwenyekiti wake wa Taifa, vyombo vya chama na Mabaraza ya chama.

**41. NAIBU KATIBU MKUU.**

(a) Atamsaidia katibu mkuu katika shughuli zake za kila siku katika chama.

(b) Atakaimu majukumu ya katibu atakapokuwa hayupo.

**42. WAKUU WA KURUGENZI.**

(a) Kurugenzi zote zitakuwa chini ya ofisi ya katibu mkuu.

(b) Pamoja na majukumu yao ya kila siku watawajibika kwa katibu mkuu.

(c) Watakuwa wafuatiliaji na kutoa tathmini kwa katibu mkuu.

## SEHEMU YA KUMI

## BODI YA WADHAMINI

**43. BODI YA WADHAMINI WA CHAMA.**

(a) Kutakuwa Bodi ya wadhamini wadhamini ya chama.

(b) Bodi itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (5)

## 44. NAMNA YA KUIPATA BODI YA WADHAMINI WA CHAMA.

i. Mwenyekiti na Katibu wa Bodi watachaguliwa na mkutano mkuu Taifa

ii. Wajumbe wengine watatu(3) wataeuliwa na Kamati Kuu ya Utendaji

iii. Uongozi wa Baraza hili la wadhamini utazingatia uwakilishi wa Bara na Zanzibar (***Muungano***)

## 45. MAJUKUMU YA BODI YA WADHAMINI WA CHAMA.

(a) Bodi ya Wadhamini wa chama itakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Wenye mamlaka ya kufungua na kufuta kesi yoyote inayohusu chama

ii. Kulinda na kusimamia Mali na Fedha zote za chama.

iii. Watabeba Dhamana nzima ya chama, watakuwa na uwezo wa kisheria wa kuhoji, kuchunguza na kutoa maamuzi sahihi kwa suala lolote linalohusiana na mali ama Fedha za chama

iv. Watapokea Ruzuku,Misaada,kukopa au kukopesha watakapoona kuna manufaa kwa ustawi wa chama

v. Kutoa ushauri wowote wa Busara pale itakapooona kuna ambo hayaendi sawa kwa lengo la kuimarisha kazi,ustawi na ushindi wa chama.

vi. Kutafuta Wafadhili na wadhamini wa shughuli za chama

# SEHEMU YA KUMI NA MOJA

# FEDHA ZA CHAMA.

## 46. VYANZO VYA FEDHA ZA CHAMA.

Vyanzo vya fedha vya chama vitajumuisha:-

(a) Ruzuku ya Serikali,Ada na viingilio vya wanachama ambavyo viwango vyake kufuatana na thamani ya fedha vitapangwa na kamati kuu ya utendaji.

(b) zawadi , misaada, ahadi, ufadhili na wakfu.

(c) Pato halisi litakalotokana na machapisho na vitu vingine vinavyouzika.

(d) Mapato yatakayotokana na vitega uchumi vya chama kama vitakavyopitishwa kamati kuu ya utendaji

(e) masuala yote yanayohusu Fedha za chama yatasimamiwa na Bodi ya Wadhamini wa chama.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## MIIKO YA CHAMA.

### 47. MIIKO NDANI YA CHAMA.

(a) Miiko ni makatazo yote yasiyostahili kufanywa na kiongozi ,miiko ipo mingi lakini wa shughuli za kisiasa ,kiongozi ama mwanachama wa NRA hutakiwi kufanya yafuatayo;

i. Kutoa kauli inayohusu msimamo wa chama bila ya idhini ya mwenyekiti Taifa na vikao halali vya chama kwenye vyombo vya habari, mkutano wa hadhara na kwengineko.

ii. Kuhujumu mali za chama ama za umma kwa makusudio ya kujinufaisha binafsi,kuomba rushwa ama kutoa rushwa

iii. Kutumia lugha ya matusi, kashfa kwa viongozi wa chama, wanachama na viongozi wa Serikali.

iv. Kutowajibika, kukwepa majukumu bila sababu ya msingi

v. Kufitinisha, kufarakanisha, kuleta majungu ndani na nje chama.

vi. Kuhatarisha amani ndani na nje ya chama, kwa Serikali iliyoko madarakani na nchi kwa ujumla.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### 48. ADHABU ZA UKIUKAJI WA MIIKO NDANI YA CHAMA.

(a) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa sehemu ya kumi na Mbili,ibara ya 47(a)(i). **Adhabu** ,kama mkosaji ni kiongozi anastahiki kuvuliwa madaraka yake mara moja pindi itakapothibitika. Kama ni mwanachama wa kawaida ataonywa kwa maandishi mara mbili,na mara ya tatu atavuliwa uwanachama wake.

(b) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa ibara ya 47(a)(ii), **Adhabu** yake ni kufukuzwa uwanachama au kushitakiwa mahakamani kwa kibali cha kamati kuu ya utendaji ama vyote kwa pamoja.

(c) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa ibara ya 47(a)(iii) , **Adhabu** yake ni kuonywa mara tatu na mara ya nne kusimamishwa uongozi na kamati kuu.

(d) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa ibara ya 47(a)(iv) **Adhabu** yake ni kuonywa mara tatu,mara ya nne kamati kuu itamvua madaraka yake mara moja.

(e) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa ibara ya 47(a)(v) **Adhabu** yake ni kufukuzwa uanachama haraka iwezekanavyo kwa manufaa ya chama.

(f) Hukumu ya makosa yaliyoelezwa ibara ya 47(a)(vi) **Adhabu** yake ni kufukuzwa uanachama haraka iwezekanavyo kuripotiwa katika vyombo vya kisheria ili kukinusuru chama.

### SEHEMU YA KUMI NA NNE.

## USULUHISHI NDANI YA CHAMA.

**49. USULUHISHI.**

(a) Mabishano ya aina yoyote migogoro ,mafarakano au kuhusu ufafanuzi wa katiba hii au yote yanayowahusisha wanachama,chama na wanachama au mwanachaa kwa mwanachama mwingine au mabishano yoyote kuhusu mambo ya chama yataamuliwa kwa njia ya usuhishi utakaosimamiwa na Baraza la Wazee la Chama na Bodi ya Wadhamini wa chama.

(b) Maamuzi ya vyombo hivi yataheshimiwa na wanachama wote

### SEHEMU YA KUMI NA TANO.

### NYONGEZA YA KATIBA

**50. NYONGEZA.**

(a) katiba hii itakuwa ndio muongozo na haitapingana na Katiba mama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Kwa mujibu wa katiba hii utaratibu, shabaha na matayarisho ya kuanzishwa kwa chama hiki yameoneshwa ingawaje kwa ufupi na kwamba marekebisho na mabadiliko ya mara kwa mara yanaweza kufanyika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ,kisayansi ,kiteknolojia na kijamii ili mradi kufanya hivyo hakutakwenda kinyume na katiba hii na katiba ya nchi.

(c) Marekebisho yoyote yatafanyika kwa idhini ya Mkutano mkuu wa Taifa.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA.

## ORODHA

### 51. ORODHA YA WAJUMBE WA BODI YA WADHAMINI;

MAJINA YA WAJUMBE WA BODI YA WADHAMINI WA CHAMA KWA MWAKA

**(2017-2022)**

| S/N | JINA KAMILI | CHEO | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1 | **MOHAMED ISMAIL ABOOD** | MWENYEKITI | |
| 2 | **KHAMIS ALLY HASSAN** | KATIBU | |
| 3 | **RASHIDI SAIDI NYUMBA** | MJUMBE | |
| 4 | **SALIM ALI MAHFOUDH**<br>ALLY SALIM MAHFOUDH | MJUMBE | |
| 5 | **HALIMA JUMA RAJABU** | MJUMBE | |

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **MWENYEKITI TAIFA** | **KATIBU MKUU TAIFA** |
| **SIMAI A. ABDULLAH** | **HASSAN K. ALMAS** |